# Mtume Wa Mwisho صلى الله عليه وسلم





Sheikh-e-Tariqat, Amir-e-Ahl-e-Sunnat
Muasisi wa Dawat-e-Islami, Allamah Maulana Abu Bilal
**MUHAMMAD ILYAS**
**Attar Qadiri Razavi**

سب سے آخِری نبی ﷺ

**Sab Say Aakhiri Nabi ﷺ**

# MTUME WA MWISHO ﷺ

*Ilitafsiriwa kwa kiswahili na:*

**Idara ya Tafsiri (Dawat-e-Islami)**

www.dawateislami.net

**Mtume wa mwisho ﷺ**

Tafsiri ya Kiswahili ya 'Sab Say Aakhiri Nabi ﷺ'

◈

**HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA**

Hakimiliki © 2023 Maktaba-tul-Madinah

Hairuhusiwi kunakili, au kusambaza sehemu yoyote ya chapisho hili kwa namna yoyote au kwa njia yoyote ile, kielektroniki, mitambo, kunakili, kurekodiwa au vinginevyo, bila ya idhini ya maandishi ya Maktaba-tul-Madinah.

| | |
|---|---|
| **Chapisho la kwanza:** | Ẓul-Qa'daĥ, 1444 AH – (May, 2023) |
| **Imetolewa na:** | Idara ya tafsiri (Dawat-e-Islami) |
| **Mchapishaji:** | Maktaba-tul-Madinah |
| **Idadi:** | - |

## Ufadhili

Tafadhali kuwa huru kuwasiliana nasi ikiwa ungependa kufadhili uchapishaji wa kitabu cha kidini au kijitabu kwa ajili ya kuwafikishiya SWADAKA YA MILELE familiya yako waliyokufa.

**Maktaba-tul-Madinah**

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah Mahallah Saudagran, Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

✍ Anuani: maktabaglobal@dawateislami.net - maktaba@dawateislami.net

✆ **Simu:** +92-21-34921389-93 – 34126999

💻 **Tovuti:** www.dawateislami.net

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ
اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

# *Du'a ya kusoma kitabu*

Soma Du'a ifuatayo (dua) kabla ya kusoma kitabu cha dini au somo la Kiislamu, utakumbuka chochote unachosoma, اِنْ شَآءَ اللّٰه:

اَللّٰهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَانْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَـا ذَا الْجَلَالِ وَالْاِكْرَام

## Tafsiri

*Ewe Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ! Tufungulie milango ya elimu na hekima, na utumiminie sisi Sikitiko/Ruhuma zako! Ewe mwenye utukufu na heshima zaidi!* *(Al-Mustatraf, juzuu 1, ukurasa 40)*

**Kumbuka:** Mswaliye Mtume Mtukufu صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَسَلَّم mara moja kabla na baada ya Du'a.

# Jedwali la Yaliyomo


Mtume wa mwisho ﷺ ........ 1
Ubora wa kumswalia Mtume ........ 1
Sayyiduna Jibril عَلَيْهِ السَّلَام anasema Salam (hadithi) ........ 1
اَلْحَمْدُ لِلّٰه Sisi ni Ummat wa Mtume wa mwisho ﷺ ........ 3
Wajibu muhimu zaidi ........ 4
Maana ya Khaatam ........ 5
Hata Wanyama wanamwamini Mtume wa mwisho ﷺ ........ 6
Ufafanuzi wa ushairi wa Raza ........ 7
Hakuna Dalili itakayo ulizwa ........ 9
Inakuwaje kuomba miujiza kwa nabii wa uongo? ........ 9
لَا نَبِيَّ بَعْدِيْ ........ 10
Hasara ya kutojali ulinzi wa Imani ........ 10
Kutojali Imani kunatisha ........ 11
Muumin asubuhi, kafiri jioni ........ 12
Ufafanuzi wa hadithi ........ 12
Hadithi isiyo ya kawaida ya Mtakatifu aliyefichwa ........ 14
Kifo chenye kuburudisha imani (mfano wa Madani) ........ 18
Ufafanuzi wa ushauri wa Raza ........ 20
Ubora wa kupitisha Ahadith 40 (arubaini) ........ 21
Hadithi 40 kuhusu Imani ya Utume ........ 21
Matofali ya mwisho ya jumba la mwanga ........ 21
Ufafanuzi wa hadithi ........ 22
Maana ya Khaatam-un-Nabiyyeen ........ 23
Fadhila sita ........ 24

Ufafanuzi wa hadithi ........ 24
Mimi ni Aqib........ 26
Kiongozi wa Manabii wote........ 26
Ufafanuzi wa Hadithi ........ 27
خَاتَمُ النَّبِيِّيْن........ 27
Maana ya Aakhir-ul-Masajid ........ 27
Ingia Peponi ........ 28
Hakuna Nabii mwingine kabisa baada yangu........ 28
Maelezo ya Hadithi........ 28
Ummah wa kwanza kuingia Peponi........ 30
Mazungumzo mafupi, yenye manufaa ........ 31
Sababu ya kuwa Nabii mkubwa kuliko Manabii wote (hadithi)........ 31
Maelezo ya Hadithi........ 33
Kutakuwa na Manabii wa uongo 30 (thelathini) ........ 33
Maelezo ya Hadithi........ 33
Ubora wa Maula Ali........ 34
Maelezo ya Hadithi........ 35
Umesema ukweli........ 36
Tafsiri ya ndoto ........ 36
Nur (mwangaza) watakimbia mbele yao........ 37
Viumbe vyote vitamwita Mtume wa Mwisho Siku ya Hukumu........ 38
Kama Muhammad asingekuwepo, nisingekuumba wewe ........ 38
Imetajwa katika Taurati........ 40
Wa kwanza na wa mwisho ........ 41
Nabii wa kwanza na wa mwisho ........ 41
'اَنَا لَهَا' Itaandikwa kwenye midomo ya Huzoor wangu ........ 43
Ufafanuzi wa mashairi ya Hassan........ 43

I hid nothing, but... (an anecdote) ... 44
Maneno Matano ya Maswahaba na Taba'een ... 45
1. Uandishi kati ya mabega yote mawili ... 45
2. Kama asingekuwepo, hakuna kitu kingekuwapo ... 46
Ufafanuzi wa ushairi wa Raza's ... 46
3. Ujumbe kwa Hadhrat Ibrahim عَلَيۡهِ السَّلَام ... 47
Ufafanuzi wa ushairi wa Raza's ... 48
4. Ufunuo juu ya Sayyiduna Ash'iya عَلَيۡهِ السَّلَام ... 48
Maelezo ya Ufalme wa Syria ... 49
5. Uteremsho juu ya Sayyiduna Yaqoob عَلَيۡهِ السَّلَام ... 50
Kauli mbiu za mwisho wa Utume ... 51
Mpe mtu mwingine kijitabu hiki baada ya kukisoma ... 53

# Mtume wa mwisho ﷺ

Ewe Mola wa Mustafa! Yoyote anayesoma au kusikiliza kijitabu hiki cha kurasa 53, 'Nabii wa Mwisho صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم', msamehe kikamilifu na mfanye jirani bora wa Mtume Mtukufu صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم katika Jannat-ul-Firdaus.

اٰمِيْن بِجَاهِ النَّبِيِّ الْاَمِيْن صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

## Ubora wa kumswalia Mtume

Enyi watu! Hakika mwenye kupata kuokolewa kwa haraka Siku ya Qiyama kutokana na magumu yake na uwajibikaji wake ni yule miongoni mwenu ambaye ameniswalia kwa wingi duniani. *(Al-Firdaus bima Soor-ul-Khittab, juzuu ya 5, uk. 277, Hadithi 8175)*

## Sayyiduna Jibril عَلَيْهِ السَّلَام anasema Salam (hadithi)

Mtume Mtukufu صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: Jibril (عَلَيْهِ السَّلَام) akaja akaniambia Salam hivi: 'اَلسَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ظَاهِرُ، اَلسَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَاطِنُ' Nikasema, 'Ewe Jibril! Hizi ni sifa pekee za Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani zinamfaa Yeye pekee. Inakuwaje zinahusiana na binadamu kama mimi?' Jibril alisema, 'Mwenyezi Mungu Mtukufu amekutukuza kutokana na sifa hizi, amekunyanyua juu ya Manabii na Mitume kutokana na (sifa hizi), na akaleta

jina lako na sifa zako kutoka kwa jina lake na sifa zake. Mwenyezi Mungu Mtukufu amekuita ‘Awwal’, kwani wewe ni wa Mwanzo wa Mitume wote kwa upande wa uumbaji. Amekuita ‘Aakhir’, kwani ni mwenye kuja mwisho baada ya zama za Mitume wote, na wewe ni Mtume wa Mwisho wa Umma wa mwisho. Mwenyezi Mungu Mtukufu alikuita ‘Batwin’, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu aliandika jina lako pamoja na jina lake kwa ajili ya kubaki milele kwa Nur ya dhahabu kwenye mguu wa ‘Arsh (kiti cha enzi) miaka elfu mbili kabla ya kuumbwa Sayyiduna Adam عَلَيْهِ السَّلَام. Kisha akaniamrisha kusoma Swalat juu yako, basi nikasoma Swalat kwa muda wa miaka elfu moja na Salam kwa miaka elfu moja mpaka Mwenyezi Mungu Mtukufu akakutuma wewe kuwa ni Mtume mwenye Kubashiri na kuonya, na mwitaji kumuendea Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa idhini yake na jua lenye kung’arisha. Na Mwenyezi Mungu Mtukufu akakuita 'Zaahir' kwa kuwa amejaalia dini yako iwe ni yenye kughilibu dini zote na akadhihirisha Sheria yako na ubora wako kwa wote wanaoishi ardhini na mbinguni. Basi hakubaki yeyote isipokuwa amekuswalia. Mwenyezi Mungu Mtukufu atume rehema juu yako! Hivyo, Mola wako ni Mahmoud (yaani, mwenye kuhimidiwa) na wewe ni ‘Muhammad’ (yaani, mwenye kusifiwa sana). Mola wako ni ‘Awwal wa Aakhir na Zaahir wa Batwin’, na (kwa kujaaliwa na yeye Mwenyezi Mungu Mtukufu) wewe pia ni ‘Awwal wa Aakhir na Zaahir wa Batwin’.’ Mtukufu

Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم (aliposikiliza) akasema: Sifa njema zote njema ni za Mwenyezi Mungu Aliyeninyanyua juu ya Manabii wote mpaka akajaalia ubora kwenye jina langu na sifa zangu pia.' *(Shar' Al-Shifa'-lil-Qaari, juzuu ya 1, uk.515; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 663)*

## اَلْحَمْدُ لِلّٰه Sisi ni Umma wa Mtume wa mwisho ﷺ

Enyi wafuasi wa Mtume wa Mwisho! Mwenyezi Mungu Mtukufu alitufanyia wema mkubwa sana kwamba akatufanya kuwa Ummati wa Kipenzi chake Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم.

اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ Mtume mtakatifu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ndio Mtukufu kuliko Mitume wote na Manabii wote. Na kwa rehema za Mwenyezi Mungu Mtukufu, Ummah wake ndio umma bora kuliko Umma wote waliyotangulia kwa baraka ya Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم.

*Saaray Rasoolon say tum bar-tar, tum saaray Nabiyon kay Sarwar*
*Sab say behtar Ummat waalay,* صلّی اللّٰہ علیک وسلّم

*(Saman-e-Bakhshish, uk. 93)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد ﷺ

## Wajibu muhimu zaidi

Enyi wafuasi wa Mtume Mtukufu! Kumuamini Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kama Mtume wa Mwisho wa Mwenyezi Mungu Mtukufu ni moja ya mahitaji ya Dini. Yeyote anayeikanusha au kujishuku hata kidogo, huyo ni Kafir na murtadi (yuko nje ya Uislamu). Mwenyezi Mungu Mtukufu amesema katika Juzuu ya 22, Surah Ahzab, Aya ya 40:

مَا كَانَ مُحَمَّدٌ اَبَاۤ اَحَدٍ مِّنْ رِّجَالِكُمْ وَ لٰكِنْ رَّسُوْلَ اللّٰهِ وَ خَاتَمَ النَّبِيّٖنَؕ وَ كَانَ اللّٰهُ بِكُلِّ شَیْءٍ عَلِیْمًا۠ ﴿۴۰﴾

***Tafsiri kutoka Kanz-ul-Iman:*** *(Mtume Mpenzi) Muhammad si baba wa yeyote katika wanaume wenu, bali ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na ni wa Mwisho wa Mitume wote. Na Mwenyezi Mungu ni mjuzi wa kila kitu.*

*Ufafanuzi wa Ayah Kuhusiana na sehemu hii 'وَخَاتَمَ النَّبِيّٖنَ' wa Ayah, Hadhrat 'Allamah Maulana Syed Muhammad Na'eem-ud-Deen Muradabadi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameandika katika 'Khazain-ul-Irfan': Yaani, Muhammad Mustafa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ni Mtume wa Mwisho, kwani hakuna Nabii mwengine atakayekuja baada yake, na Utume umemfikia mwisho wake, na hakuna awezaye kupata utume baada ya utume wake mpaka Sayyiduna Isa* عَلَيْهِ السَّلَام

*atakaposhuka. Na yeye (Sayyiduna 'Isa عَلَيْهِ السَّلَام) pia ingawa tayari amepata utume, lakini atafuata Sharia ya Mtume Muhammad baada ya kushuka na atahukumu kwa mujibu wa Sharia hii, na kuswali kuelekea Qiblah cha Mtume Mtukufu yaani, Al Ka'bah. (Kumbukeni!) Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kuwa kwake Mtume wa Mwisho ni jambo lililothubutu wazi kabisa katika Ayah iliyo wazi kabisa ya Qur'ani Tukufu, na Hadithi ambazo zimefikia kiwango cha Tawatur (yenye wapokeaji wengi katika kila zama). Haya yote yamethibitisha kuwa Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ni Nabii wa Mwisho, na hakuna Nabii mwengine atakayekuja baada yake. Yoyote anayeona kuwa inawezekana kwamba mtu yoyote anaweza kupokea utume baada ya utume wa Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, huyo ni kafiri na mkanushaji wa Muhuri wa Utume, na yuko nje ya Uislamu.* *(Khaza'in-ul-'Irfan, Uk. 763; Sirat-ul-Jinan, juzuu ya 8, Uk. 47, muhtasari)*

## Maana ya Khaatam

Al-Haaj Mufti Ahmad Yaar Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameandika: '*Khaatam*' inatokana na Khatm, na Khatm maana yake ni muhuri na mwisho. Kwa hakika, muhuri unaitwa Khaatam, kwasababu inawekwa kwenye mwisho wa mada yoyote na ukiwekwa juu ya mfuko (au chombo) basi hakuna chochote

kilichoko ndani yake kinachoweza kutoka nje na chochote cha nje kinachoweza kuingia ndani. Vile vile, muhuri huu umeshawekwa; Ua la mwisho la bustani ya utume limeshachanuliwa. Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم mwenyewe ameeleza maana ya Khatam-un-Nabiyyeen: ‘لَا نَبِيَّ بَعْدِیْ’ yaani, hakuna mtume mwingine baada yangu. *(Shan-e-Habib-ur-Rehman, uk. 171)*

*Ba'd Aap kay hergiz na aye ga Nabi naya*
*Wallah! Iman hay mayra, aye Aakhiri Nabi*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Hata Wanyama wanamwamini Mtume ni wa mwisho ﷺ

Imesimuliwa kutoka kwa Sayyiduna ‘Abdullah bin ‘Umar رَضِیَ اللهُ عَنْهُمَا kwamba mbedui mmoja kutoka katika ukoo wa Bani Sulaim alikuja kwa Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. na kusema, ‘Sitakuamini mpaka huyu yuru wangu akuamini.’ Baada ya kusema hivyo, alimweka yuru wake mbele yake. Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. alimuita yuru na yeye akamuitikia ‘لَبَّیْکَ وَ سَعْدَیْکَ’ (yaani, nimekuitikia na niko tayari kukutii na kufuata unayoyataka) kwa sauti kubwa huku waliyohudhuriya wote walisikia. Kisha Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akauliza, Ni nani unayemuabudu (yaani anayestahiki kuabudiwa)?” Yule yuru

akasema: “Mola wangu Mlezi ni ambaye Arsh yake iko juu mbinguni, na utawala wake uko juu ya ardhi, na rehema zake ziko Peponi na adhabu yake iko kwenye Jahannam.” Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. kisha akauliza, ‘Ewe yuru! Niambie mimi ni nani?’ Akasema kwa sauti kubwa, ‘اَنْتَ رَسُوْلُ رَبِّ الْعَالَمِيْنَ، وَخَاتَمُ النَّبِيِّيْنَ’ yaani, Wewe ni Mjumbe wa ‘اللّٰهُ رَبُّ الْعَلَمِين’ na Mtume wa Mwisho. Anayekuamini wewe kuwa ni mkweli, basi amefaulu; na atakayekukanusha, basi yeye ni mwenye hasara.’ Alipoona hivyo, mbedui alivutiwa sana na mara moja akatamka Kalimah na akawa Muislamu. *(Mu’jam Awsat, juzuu ya 4, uk. 283, Hadithi 5996)*

*Aye bala! Bay khiradi-e-kuffaar, rakhtay hayn aisay kay haq mayn inkar*

*Keh guwahi ho gar us ko darkar, bay zaban bool utha kertay hayn*

*(Hadaiq-e-Bakhshish)*

## Ufafanuzi wa ushairi wa Raza

Wale wasiomuamini Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ni wajinga sana. Hata hivyo, ikiwa Mtume wetu Mpenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم anataka kutoa ushuhuda juu ya kuwa Nabii wa Kweli na wa Mwisho, hata wanyama wasioweza kusema, n.k. wataanza kusema ili kutoa ushuhuda.

## Umuhimu wa imani katika Khatm-e-Nubuwwat (Muhuri wa Utume)

Enyi wapenzi wa Mtume wa Mwisho! Imani ya Muhuri wa Utume inakusudiwa kuamini kwamba Mtume Mustafa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ni Mtume wa Mwisho. Mwenyezi Mungu Mtukufu amemaliza mlolongo wa utume juu yake. Tangu zama za maisha dhahiri ya Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم hadi Siku ya Hukumu, hakuwezi kuwa na Nabii yoyote mpya. Baada ya kuwasili kwa Sayyiduna 'Isa عَلَيْهِ السَّلَام, haitaleta tofauti yoyote kwenye utume, kwani maana ya Khatam-un-Nabiyyin ni kwamba baada ya Zuhoor ya (kudhihiri) Muhammad Arabi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, hakuna atakayepokea utume. Sayyiduna 'Isa عَلَيْهِ السَّلَام ni nabii wa zamani. Yeye, hatahubiri Sharia yake kama Nabii, bali atahubiri tu Sharia ya Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Atakuja kama Ummati wa Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم *(Tafseer Nasfi, uk. 943).*

Kumbuka! Baada ya nabii kupokea utume, utume wake haukomeshwi, lakini kwa hakika, utume wao utabaki milele. Imeelezwa katika ukurasa wa 110-111 wa 'Fatawa Radawiyyah': 'Hasha! Nabii haondolewi utume, wala Sayyiduna 'Isa عَلَيْهِ السَّلَام hataondolewa utume, wala kuwa Ummati wa Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم haitapingana na utume." (Fatawa Radawiyyah) Daraja ya imani ya mwisho wa utume ni sawa na imani ya

Tawhid, kwa maana kwamba zote mbili zinatokana na mahitaji ya dini. Kwa hiyo, kama inavyotakiwa kwa Muislamu kuamini kwamba Mwenyezi Mungu ni Mmoja, vivyo hivyo, ni muhimu pia kwake kuamini kwamba kipenzi cha Mwenyezi Mungu Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ni Mtume wa mwisho.

## Hakuna Dalili itakayo ulizwa

Sayyiduna Imam Abu Mansur Matureedi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameandika: Yeyote anayedai kuwasili kwa nabii baada ya Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, hataulizwa dalili yoyote, bali, imani (ya mtu huyo) itakataliwa (moja kwa moja), kwasababu Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. amesema 'لَا نَبِيَّ بَعْدِیْ' yaani, hakuna nabii mwingine baada yangu. *(Tawilaat-e-Ahl-e-Sunnah, juzuu ya 8, uk. 396)*

## Inakuwaje kuomba miujiza kwa nabii wa uongo?

Sikiliza jibu lililoandikwa katika ukurasa wa 134 wa 'Malfuzaat-e-A'la Sayyiduna': Je, miujiza inaweza kuulizwa kutoka kwa Mudda'i-e-Nabuwwat (yaani, anayedai kwa uwongo kuwa nabii?)

**Jibu:** Ikiwa mtu atauliza kuonyesha miujiza kutoka kwa Mudda'i-e-Nabuwwat (yaani, anayedai kuwa Mtume) kwa kuzingatia kwamba atashindwa na uongo wake utadhihiri mbele ya watu, hakuna ubaya; na ikiwa atauliza kwa ajili ya

kupata uthibitisho iwapo anaweza kuonyesha miujiza yoyote au la, atakuwa kafiri mara moja. *(Fatawa Aalamgiri, juzuu ya 2, uk. 263, Kutoka kwa)*

## لَا نَبِیَّ بَعۡدِیۡ

A'la Sayyiduna رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Kutokana na Hadithi hii Mutawatir 'لَا نَبِیَّ بَعۡدِیۡ' yaani, hakuna Nabii mwingine baada yangu, warithi na watangulizi wote wa Ummat-e-Marhooma (yaani, Mwenyezi Mungu Mtukufu auhurumie Umma huo) daima wamekuwa wakitafsiri maana ile ile ya kwamba Mtume Mtukufu صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ni Mwisho wa Mitume wote bila ya kubainisha yeyote. Haiwezekani kabisa kwa yeyote kuupokea utume pamoja na Mtume Mtukufu صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم au baada yake mpaka Siku ya Hukumu. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya. 14, uk. 333)*

*Sab Ambiya kay ho tum-heen Sardar la-jaram*
*Tum sa nahin hay dosra aye Aakhiri Nabi*

صَلُّوۡا عَلَی الۡحَبِیۡب    صَلَّی اللّٰهُ عَلٰی مُحَمَّد

## Hasara ya kutojali ulinzi wa Imani

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Kitu cha thamani zaidi kuliko vyote kwa binadamu ni Imani yake. Kwa rehema za Mwenyezi

Mungu Mtukufu, yoyote ambaye ana neema ya Imani, ingawa ni masikini wa pesa, yeye ni tajiri zaidi kuliko milionea, bilionea ambaye amenyimwa neema ya Imani. Kwa upande mwingine, tajiri ambaye amenyimwa neema ya Imani kwa hakika ni fukara na masikini. Na 'مَعَاذَاللّٰه ثُمَّ مَعَاذَاللّٰه' yoyote atakayekufa katika hali hii (ya ukafiri) ataishi Motoni milele. Kila Muislamu anapaswa kuendelea kumuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa ulinzi wa Imani pamoja na kifo cha amani. Katika zama hizi za fitna, ambapo uvivu mkubwa katika kutenda mema umetutawala, pia kuna ukosefu mkubwa wa kuwa na wasiwasi juu ya ulinzi wa Imani. Kila siku, fitna mpya mpya za kila aina zinajitokeza na hudhoofisha Imani ya Waislamu kwa njia tofauti. Ulinzi wa Imani ni muhimu sana. Iwapo umeishi maisha yote katika mambo ya kheri, lakini (Mwenyezi Mungu asijaalie) ukanyimwa imani wakati wa kifo, itabidi uishi Motoni milele. Mtume Mtukufu akasema: 'اِنَّمَا الْاَعْمَالُ بِالْخَوَاتِيْم' yaani, 'Hakika Matendo huzingatiwa mahitimisho yake.' *(Bukhari, juzuu ya 4, uk. 274, Hadithi 6607)*

*Attar hay Iman ki hifazat ka suwali*
*Khali nahin jaye ga yeh Darbar-e-Nabi say*

## Kutojali Imani ni jambo hatari

Ni jambo la kutisha sana kwamba kama vile uzembe

unavyosababisha upotevu wa mali ya dunia inapokuja kwenye suala la usalama wake, suala la ulinzi wa Imani ni hatari zaidi. Imeelezwa katika ukurasa wa 495 wa 'Malfuzaat-e-A'la Hazrat kwamba Wanavyuoni wa Kiislamu wamesema, 'Yoyote asiye na khofu ya kunyakuliwa Imani, kuna khofu ya kutisha ya kunyakuliwa Imani yake wakati wa kutolewa roho.'

*Musalman hay Attar tayri 'ata say*
*Ho Iman per khatimah ya Ilahi*

## Muumin Asubuhi, Kafiri Jioni

Mtume wa mwisho صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: "Fanyeni haraka kutenda mema kabla ya fitna hizo ambazo ni kama sehemu za usiku wa giza. Mtu angekuwa Muumini asubuhi na jioni anakuwa kafiri, na jioni anakuwa Muumini na asubuhi atakuwa kafiri. Zaidi ya ziada, atauza dini yake kwa faida ya kidunia.' *(Muslim, uk. 69, Hadithi 313)*

## Ufafanuzi wa hadithi

Kuhusiana na Hadithi hii, Sayyiduna Imam Sharaf-ud-Deen Nawawi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه, mfasiri wa Muslim, amesema: Katika Hadithi hii, tumesukumwa kufanya mambo mema kabla haujafika wakati tushindwe kufanya jambo jema kama hilo kwasababu ya

kushughulishwa na fitna hizo zinazofuatana ambazo zitaongezeka zaidi kama vile giza linavyotanda katika usiku wa giza sana ambao hata mwezi hauwezi kuonekana. Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ameeleza aina moja ya fitna hizo kali hapa, na fitna hizo zitakuwa kali sana kiasi kwamba moyo wa mwanadamu utabadilika siku moja, na huku ni kubadilika kubwa sana. *(Sharah Muslim-lil-Nawawi, juzuu ya 2, uk. 133)*

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Ni bahati mbaya iliyoje mtu kuuza Imani yake kwa starehe za kawaida na anasa za ulimwengu wa muda mfupi, مَعَاذَاللّٰه anafanya biashara ya Imani na Kufru, na kuufanya Moto wa Jahannamu kuwa makazi yake badala ya Pepo. Wapenzi wote wa Mtume Mtukufu lazima waombe Du'a hii ya Masnun 'يَا مُقَلِّبَ الْقُلُوْبِ ثَبِّتْ قَلْبِيْ عَلٰى دِيْنِكَ' yaani, Ewe Mbadilishaji nyoyo! Uimarishe moyo wangu katika Dini Yako.' Kwa Baraka ya Mtume Mpenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, Mwenyezi Mungu Mtukufu aiweke salama Imani yetu, atujaalie tuwe imara katika Dini ya Kiislamu, na atujaalie tufe shahidi kwa Imani huku tukimuona Mtume kipenzi. صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم (wakati wa kutolewa roho) chini ya kivuli cha kuba la Kijani, na kuzikwa Jannat-ul-Baqi', na atujaalie kuwa majirani nae huko Jannat-ul-Firdaus!

اٰمِين بِجَاهِ خَاتَمِ النَّبِيّين صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

*Hayn Ghulam Aap kay jitnay, karo door un say fitnay*
*Burri Maut say bachana, Madani Madinay walay*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Kisa cha ajabu cha Mcha Mungu aliyejificha

Wakati Swahaba wa Mtume Mtakatifu Sayyiduna Nadlah bin Mu'awiyyah رَضِىَ اللّٰه عَنْهُ, pamoja na Muhajirina 300 na Ansaar walikuwa njiani kuleta neema za vita kutoka Hulwan, Iraqi, jioni ilianguka karibu na mlima. Hivyo, Sayyiduna Nadlah رَضِىَ اللّٰه عَنْهُ alitoa Adhana. Aliposema 'اَللّٰهُ اَكْبَر اَللّٰهُ اَكْبَر', sauti ikatoka mlimani. Mtu fulani alikuwa akisema, 'Ewe Nadlah! Umetaja ukuu wa Mkuu!' Aliposema 'اَشْهَدُ اَنْ لَّآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰه', jibu likaja, 'Ewe Nadlah! Umeitaja Tawhid safi. Aliposema 'اَشْهَدُ اَنَّ مُحَمَّدًا رَّسُوْلُ اللّٰه', ikasikika sauti, 'Ametumwa kama Nabii hivi kwamba hakuna nabii baada yake. Yeye ndiye anayetoa maonyo. Yeye ndiye ambaye habari njema kuhusu yeye ilitolewa na Sayyiduna 'Isa عَلَيْهِ السَّلَام . Mwishoni mwa Ummah wake, Siku ya Qiyama itatokea.' Wakati swahaba wa Mtume Mtukufu Sayyiduna Nadlah رَضِىَ اللّٰه عَنْهُ alisema 'حَيَّ عَلَى الصَّلٰوة', jibu likaja, 'Swala ni faradhi, habari njema ni kwa mwenye kuiendea na akaidumisha.' 'حَيَّ عَلَى الْفَلَاح' iliposemwa ikasikika sauti: 'Amefaulu aliyekuja kwa ajili ya Swalah na akashikamana nayo. Amefaulu aliyemtii Mtume Mtukufu صَلَّى اللّٰه عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم.' Aliposema 'اَللّٰهُ اَكْبَر اَللّٰهُ اَكْبَر، لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰه', sauti ikaja,

'Umepata Ikhlas kamili, hivyo kutokana na hili, Mwenyezi Mungu Mtukufu ameujaalia mwili wako kuwa ni Haraam juu ya Jahannam.' Sayyiduna Nadlah رَضِىَ اللهُ عَنْهُ akasimama baada ya Swalah na kusema, 'Ewe mwenye kusema kwa uzuri! Je, wewe ni malaika, jini au Rijal-ul-Ghaib (yaani, binadamu ambaye amefichwa machoni)? Jitokeze mbele yetu na uzungumze nasi, kwani sisi ni wawakilishi wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na Mtume Wake صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم na Sayyiduna Umar رَضِىَ اللهُ عَنْهُ.' Aliposema hivyo, mtakatifu mwenye uso mzuri na ndevu nyeupe alionekana kutoka mlimani. Alikuwa amevaa shela ya sufu nyeupe. Alipofika, alisema Salam: 'اَلسَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللّٰهِ وَبَرَكَاتُهٗ' Waliohudhuria wote walijibu. Sayyiduna Nadlah رَضِىَ اللهُ عَنْهُ akasema, 'Mwenyezi Mungu Mtukufu akurehemu, wewe ni nani?' Akasema, 'Mimi ni Zuraib bin Sarmala.' Nabii wa Mwenyezi Mungu Mtukufu 'Isa عَلَيْهِ السَّلَام alinifanya nibaki kwenye mlima huu na akaniombea nibaki hai mpaka atakapokuja mara ya pili kutoka mbinguni.' Imeelezwa katika riwaya nyingine kwamba aliuliza, 'Yuko wapi Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم?' Sayyiduna Nadlah رَضِىَ اللهُ عَنْهُ akasema, 'Alifariki dunia.' Juu ya hili, mtakatifu alilia sana. Kisha akasema, 'Ni nani aliyemrithi?' Ikasemwa, '(Sayyiduna) Abu Bakr (Siddiq رَضِىَ اللهُ عَنْهُ).' Akauliza, 'Yuko wapi?' akajibiwa, '(Yeye pia) amefariki.' Akasema, 'Ni nani aliyemfuatia?' Akaambiwa, '(Sayyiduna) Umar رَضِىَ اللهُ عَنْهُ.' Akasema, 'Mpe Salamu yangu Amir-ul-Mu'mineen Sayyiduna Umar رَضِىَ اللهُ عَنْهُ na sema: Ewe Umar!

Weka utawala sawa, Pata ukaribu na watu, Siku ya Hukumu imekaribia. Na Ewe Umar! Mambo haya yanapojitokeza katika Umma wa Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, kuondoka duniani itakuwa bora zaidi. (Baadhi yao ni kama yafuatavyo: )

1. Wakati watu wanaanza kubadilisha Nasaba zao (yaani, kujiita Sayyid, Swiddiqi, Alawi, n.k. licha ya kutokuwa na asili.)
2. Wazee hawana mapenzi na watoto wao.
3. Watu hawaitani kwenye haki wala hawakatazani maovu.
4. Wanapata elimu (ya dini) kwa ajili ya kupata mali ya dunia.
5. Mvua hunyesha sana.
6. Watoto wanazingatiwa kuwa uzito.
7. Watu wanaanza kupamba Misikiti, lakini haina wenye kuswali.
8. Rushwa inakuwa kawaida.
9. Majengo yenye nguvu yanaanza kujengwa.
10. Watu hufuata matamanio.
11. Wanaanza kuuza Dini kwa ajili ya ulimwengu.

12. Kukata mahusiano na jamaa inakuwa kawaida.
13. Maslahi yanaenea kwenye nafsi zao.
14. Kuwa tajiri inakuwa sababu ya kuheshimika.

Mambo haya yote yatakapokuwa ya kawaida, jificheni kwenye pango ya mlima, na kujishughulisha na Dhikri ya Mwenyezi Mungu Mtukufu katika maficho hayo.' Baada ya kusema hivyo, mtakatifu huyo alitoweka.

Sayyiduna Nadlah رَضِیَ اللهُ عَنْهُ aliandika tukio hili lote na kutuma kwa swahaba wa Mtume Mtukufu Sayyiduna Saad bin Abi Waqas رَضِیَ اللهُ عَنْهُ, ambaye aliandika zaidi kwa Ameer-ul-Mu'mineen Sayyiduna Umar Farooq-e-A'zam رَضِیَ اللهُ عَنْهُ.Kwa kujibu, Sayyiduna Farooq-e-A'zam رَضِیَ اللهُ عَنْهُ aliamuru Sayyiduna Saad bin Abi Waqas رَضِیَ اللهُ عَنْهُ kwamba awachukue Muhajirina na Answaar maswahaba pamoja naye hadi kwenye mlima huo na kusali Salamu yake ikiwa mtakatifu huyo atatokea mara nyingine tena. Sayyiduna Saad bin Abi Waqas رَضِیَ اللهُ عَنْهُ alichukua Muhajirina elfu nne na maswahaba wa Answaar pamoja naye kwenye mlima ule na akatoa Adhan mfululizo kwa muda wa siku 40 (arobaini), lakini hakuna sauti au jibu lililotoka. *(Tareekh-e-Baghdad, juzuu ya 10, uk. 254; Dalail-un-Nubuwwah-lil-Bayhaqi, juzuu ya 5, uk. 425-427; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 10, uk. 691, Muhtasari)*

Mwenyezi Mungu Mtukufu atuhurumie wote na atusamehe bila ya kuwajibishwa kwa baraka yao!

اٰمِيْن بِجَاهِ النَّبِيِّ الْاَمِيْن صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

*Sab Sahabah ka hay yeh 'Aqeedah aṯal*
*Hayn yeh Khayr-ul-Wara Khatam-ul-Ambiya*

## Kifo Chenye kukuza Imani (Mfano Wa Madani)

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Ili kufikia uthabiti katika imani ya mwisho wa utume na kuweka mawazo ya umuhimu wa ulinzi wa Imani, daima kubaki kuhusishwa na mazingira ya kidini ya Dawat-e-Islami, harakati ya wapenzi wa Rasul اِنْ شَآءَاللّٰهُ الْكَرِيْم Utapokea baraka kama hizo hivi kwamba uzima na vifo vitakuwa vya fahari. Ili kuongeza shauku yako, mfano wa Madani ni kama ifuatavyo:

Ndugu wa Kiislamu yaani, Muhammad Wasim Attari, angekuja kwa Sag-e-Madinah. Maskini alipata saratani katika mkono wake wa kushoto na madaktari wakaukata mkono huo. Ndugu mwingine wa Kiislamu kutoka eneo lake alimfahamisha Sag-e-Madinah kwamba ndugu Waseem alikuwa akiteseka sana kutokana na maumivu makali. Nilifika hospitali kumtembelea. Nilimtuliza kwa kumwambia hivi: Mkono wa kushoto ulikatwa,

usijali kuhusu hilo. اَلْحَمْدُ لِلّٰه Mkono wa kulia ni salama, na neema kubwa zaidi ni kwamba اَلْحَمْدُ لِلّٰه 'Iman' pia iko salama. اَلْحَمْدُ لِلّٰه Nilimwona akiwa mvumilivu sana. Aliendelea kutabasamu hadi alipoinuka kitandani kwake na kutoka nje kuniaga. Maumivu ya mkononi yaliisha taratibu, lakini maskini alipata shida tena, ambayo ni kwamba maji yalijaa kifuani mwake. Siku zilianza kwenda kwa maumivu makali sana, Hatimaye, siku moja maumivu yaliongezeka zaidi. Alianza kuleta Dhikr ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, Chumba kilinguruma kwa sauti ya dhikri. Hali yake ilikuwa mbaya sana juhudi zilifanyika kumpeleka kwa daktari, lakini alikataa katakata. Bibi alichukua (kichwa chake) kwenye mapaja yake kwa upendo na mapenzi. Kalimah Tayyibah لَآ اِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم) ilitiririka kutoka kwenye ulimi wake, na karibu umri wa miaka 22 Muhammad Wasim aliaga dunia. اِنَّا لِلّٰهِ وَاِنَّآ اِلَيْهِ رٰجِعُوْنَ Alipokuwa karibu kuchukuliwa kwa Ghusl/kuoshwa, ghafla shuka liliondolewa usoni mwake. Uso wa marehemu ulikuwa unang'aa kama ua. Baada ya Ghusl, uso uling'aa zaidi. Baada ya mazishi, wakati wapenzi wa Rasul walipokuwa wakisoma Qasida, harufu nzuri ilianza kutoka kaburini. Hata hivyo, yeyote aliyenusa, alinusa. Mwanafamilia mmoja alimuota marehemu Muhammad Wasim Attari baada ya kifo akiwa ndani ya chumba kilichopambwa kwa maua na kuuliza, 'Unaishi wapi?' Akaashiria kwa mkono kuelekea chumba kimoja na akasema,

'Hapa ni nyumbani kwangu. Nina furaha sana hapa.' Kisha akajilaza kwenye kitanda kilichopambwa. Babake marehemu alijikuta katika ndoto akiwa amesimama karibu na kaburi la Wasim Attari. Mara moja, kaburi likapasuka na marehemu akiwa amevaa 'Imamah/Kilemba kichwani na sanda nyeupe akatoka. Aliongea kidogo na kuingia kaburini tena, na kaburi likajifunga kama awali.

Mwenyezi Mungu Mtukufu atuhurumie/atusikitikie sote na atusamehe bila ya kuwajibishwa kwa baraka yao!

اٰمِيْن بِجَاهِ النَّبِيِّ الْاَمِيْن صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

*Tau nay Islam diya tau nay jama'at mayn liya*
*Tau kareem ab koyi phirta hay 'attiyyah tayra*

## Ufafanuzi wa ushairi wa Raza

Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Ulitupa zawadi katika sura ya Uislamu na ukatuingiza katika Ummah wako. Wewe ni Mwenye Rehema. Baada ya kutoa, unaweza hata kuchukua zawadi ya Dini ya Kiislamu? (Hapana kabisa)

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Ubora Wa Kuwasilisha Hadith 40 (Arobaini)

Amesema Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم Mtume wa Mwisho, "Yoyote ambaye atahifadhi Hadith 40 kuhusu Dini kwa ajili ya kuzifikisha kwa Umma wangu, Allah عَزَّوَجَلَّ atamfufua kesho siku ya Qiyama kama mwanachuoni na mimi nitakuwa muombezi wake na shahidi wake siku ya Qiyama." *(Shuabul Imaan juz.2, uk.270, Hadith. 1726 )*

Hadithi hii inakusudiwa kuwasilisha Hadith 40 kwa watu hata kama hajaweza kuzihifadhi. *(Ashi'a-tul-Lam'aat, juzuu ya 1, uk. 186)* Kwa nia ya kupata ubora uliotajwa katika Hadith, Hadith 40 kuhusu Mtume Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kama Mtume wa Mwisho zinatajwa kama ifuatavyo:

# Hadithi 40 kuhusu Imani ya Mwisho wa Utume

## Tofali la mwisho la jumba la mwanga

1. Mfano wangu na wa manabii wengine kabla yangu ni ule wa mtu aliyejenga nyumba nzuri sana lakini akaacha sehemu ya tofali moja kwenye kona. Watu walianza kuizunguka na kuishangaa wakisema kwa nini hakuweka tofali. Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kisha akasema: 'Mimi

ndiye tofali (la mwisho) na Mwisho wa Manabii.’ *(Bukhari, juzuu ya 2, uk. 484, Hadithi 3535)*

2. Riwaya nyingine ina maneno yafuatayo pia: ‘Mimi ndiye (mjazaji) wa mahali pa tofali hilo. Nilipokuja, nilikamilisha mnyororo wa manabii.’ *(Muslim, uk. 966, Hadithi 5963)*

*Hayn woh Qasr-e-Nubuwwat ki eent aakhiri*
*Qaul-e-Shah dana Khatam-ul-Ambiya*

## Ufafanuzi wa Hadithi

Kuhusiana na Hadithi hii, Mufti Ahmad Yaar Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameandika: سُبْحٰنَ اللّٰـه! Jinsi mfano huo ulivyo mzuri kana kwamba ‘Utume’ ni kasri ya nuru, Mitume ni matofali yake yenye kung’aa, na Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ni tofali la mwisho la jumba hilo, ambalo limekamilisha jengo hilo. Tumekuja kujua kutokana na hili kwamba Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ni Mtume wa Mwisho. Hakuna nabii yeyote katika zama zake au baada yake. Kama vile jumba hili la kifalme litakavyokamilika kwa tofali hili la mwisho na hapatakuwa na nafasi ya matofali mengine, vivyo hivyo, jumba la utume lilikamilika kutoka kwangu, sasa hakuna nafasi kwa nabii yeyote. Kumbuka kwamba Sayyiduna 'Isa عَلَيْهِ السَّلَام atakuja duniani katika kukaribia kwa Siku ya Hukumu, lakini yeye ni nabii wa zamani si nabii wa mwisho, tofali hili tayari

limeshawekwa. Zaidi ya hayo, sasa hatakuja kama Mtume (kuendeleza hukmu za sharia yake), bali atakuja kama Ummati wa Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Kumbuka kwamba mwana wa mwisho ni mwana ambaye baada yake hakuna mwana kuzaliwa. Sio lazima kwamba wana wote waliomtangulia wawe wamekufa. Maana ya Mtume Mtakatifu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kuwa Mtume wa Mwisho ni kwamba hatozaliwa Nabii yeyote katika zama zake wala baada yake. Ikiwa nabii wa zamani yupo hai (wakati wake) pia haileti tofauti. Mitume wanne bado wako hai: wawili juu ya ardhi, Sayyiduna Khidhr na Sayyiduna Ilyas عَلَيْهِمَا السَّلَام; na wawili mbinguni, Sayyiduna Idrees na Sayyiduna 'Isa عَلَيْهِمَا السَّلَام. Uhai wao haupingani na Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kuwa Mtume wa mwisho. Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ndiye kiumbe wa kwanza na Nabii wa Mwisho. *(Mir'aat, juzuu ya 8, uk. 7)*

## Maana ya Khaatam-un-Nabiyyeen

Mfasiri wa Bukhari, Mufti Sharif-ul-Haq Amjadi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه, amesema: Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم yeye mwenyewe ameeleza kwamba maana ya Khaatam-un-Nabiyyeen ni **Mwisho wa Mitume**, maswahaba pia wameeleza maana hiyo hiyo, na Umma umekubaliana kabisa juu ya hili. Kwa hiyo, ikiwa mtu atasema kwamba ni rai ya watu wa kawaida (ambao sio wanazuoni) kwamba maana ya Khaatam-un-Nabiyyeen ni Mtume wa mwisho; na hakuna ubora katika hilo; na wala

haistahiki kuwa jambo la fadhila, mtu huyo ni kafiri bila ya pingamizi yoyote. *(Nuzha-tul-Qaari, juzuu ya 4, uk. 510)*

## Fadhila sita

3. Nimepewa fadhila juu manabii wote عَلَيْهِمُ السَّلَام kwa sababu ya sifa sita:

    a) Nimebarikiwa kwa maneno yenye kukusanya maana.

    b) Nimesaidiwa kwa hofu.

    c) Nimehalalishiwa mali ya ghanima.

    d) Ardhi yote imefanyiwa kuwa ni twahara na mahali pa Swalah kwa ajili yangu.

    e) Nimetumwa (kama nabii) kwa viumbe vyote.

    f) Mlolongo wa manabii umekamilika juu yangu.

*(Muslim, uk. 210, Hadithi 1167)*

## Ufafanuzi wa hadithi

Kutaja tano au sita (fadhila) haimaanishi kuwa ndio mpaka. Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amepewa ubora katika fadhila nyingi. Katika ufafanuzi wa fadhila hii (nimebarikiwa kwa maneno ya kukusanya maana), Mufti Ahmad Yaar Khan Na'eemi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه. ameandika: Maneno ya Qur'ani Tukufu pia

ni yenye kukusanya maana, na maneno ya Mtume Mtukufu pia ni yenye kukusanya maana, ambayo yanamaanisha maneno machache, yenye maana zaidi. Tazama! Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kasema, 'Matendo yanategemea nia; Dini ni nasaha; Muumin kamili ni yule anayeacha mazungumzo yasiyo na maana na mambo yasio na faida.' Hizi ni sentensi ndogo mno lakini zimekusanya Shari'ah na Twariqah nzima.

Katika ufafanuzi wa (nimesaidiwa na hofu), Mufti Ahmad Yaar Khan Na'eemi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Maadui wanapokuja kupigana vita na mimi. Bado wakiwa mbali kwa umbali wa mwezi mmoja kutoka kwangu, mioyo yao inajaa hofu yangu. Ijapokuwa watapigana, lakini kwa kujaa hofu.

Akielezea (nimetumwa (kama nabii kwa viumbe vyote) Mufti Ahmad Yaar Khan Na'eemi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Utume na sharia ya Mtume Mtukufu imewaenea viumbe vyote, kiwe na uhai au kisicho na uhai, chenye akili au bila akili. Kuelezea (mlolongo wa manabii umekamilika juu yangu), Mufti Ahmad Yaar Khan Na'eemi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameandika: Mimi ndiye Nabii wa Mwisho, ambaye mnyororo wa utume ulikamilika juu yake, hakuna nabii katika zama zangu wala baada yangu. *(Mir'aat, juzuu ya 8, uk. 10-11)*

Mitume wanne, Sayyiduna Khidhr, Sayyiduna Ilyas, Sayyiduna Idrees na Sayyiduna 'Isa عَلَيْهِمُ السَّلَام, ambao bado hawajafariki, ni

Mitume bila ya shaka yoyote, lakini baada ya kuzaliwa Mtume wa Mwisho صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, hawata hubiri tena sheria yao.

## Mimi ni Aaqib

4. Nina majina manne. Mimi ni Muhammad; Mimi ni Ahmad; Mimi ni Maahi (yaani, mwenye kuondoa/kufuta), kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu ataondoa dhambi kupitia kwangu; Mimi ni Hashir, kwani watu watakusanyika kwa nyayo zangu (yaani, nyuma yangu Siku ya Kiyama); na mimi ni Aqib. *(Bukhari, juzuu ya 2, uk. 484, Hadithi 3532)* Imam Zuhri Taba'i رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه kasema: Aqib ni yule ambaye hakuna Mtume baada yake. *(Muslim, uk. 985, Hadithi 6107)*

*Shah-e-Ambiya hay, Khuda ka hay piyara*
*Woh Nabiyon mayn sun lo! Nabi Aakhiri hay*

*Muhammad hay Ahmad, hay Sultan-e-Bat-ha*
*Woh Nabiyon mayn sun lo! Nabi Aakhiri hay*

## Kiongozi wa Manabii wote

5. Mimi ni Kiongozi wa manabii, na sisemi kwa majisifu; Mimi ni Mwisho wa Mitume, na sisemi kwa majisifu; na mimi ndiye nitakayefanya uombezi wa kwanza, na

nimekubaliwa kuwa mwombezi wa kwanza kabisa, wala sisemi kwa majisifu. *(Daarimi, juzuu ya 1, uk. 40, Hadithi 49)*

## Ufafanuzi wa Hadithi

Katika maelezo ya sehemu hii (Mimi ni Kiongozi wa Mitume) ya Hadithi, imeelezwa katika 'Mirat': Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. ataingia Peponi mbele ya Mitume wote, na Mitume wote watamfuata. Katika suala hili, Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ni Kiongozi wa manabii. *(Mirat, juzuu ya 8, uk. 28)*

## خَاتَمُ النَّبِيِّيْن

6. Hakika mimi niliandikwa kuwa ni Khatam-an-Nabiyyeen kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu wakati Sayyiduna Adam عَلَيْهِ السَّلَام bado alikuwa anakandwa kwenye udongo wake. *(Al-Ihsan bi Tarteeb Sahih Ibn-e-Habban, juzuu ya 8, uk. 106, Hadithi 6370)*

7. Hakika mimi ndiye Mwisho wa Manabii, na Msikiti wangu ni mwisho wa Misikiti. *(Muslim, uk. 553, Hadithi 3376)*

## Maana ya Aakhir-ul-Masajid

8. Riwaya nyingine ina maneno yafuatayo: 'Mimi ni Mwisho wa Mitume, na Msikiti wangu ni mwisho wa misikiti ya Mitume.' *(Al-Firdaus, juzuu ya 1, uk. 45, Hadithi 112)* Ina maana

kwamba hakutakuwa na mtume mwingine atakayezaliwa baada ya Sayyiduna Muhammad Arabi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, wala Msikiti wa Nabii hautajengwa tena.

## Ingia Peponi

9. Enyi watu! Bila shaka yoyote, hakuna Nabii yeyote baada yangu, na hakuna Ummah baada yenu. Jihadharini! Muabuduni Mola wenu, na muswali Swalah tano, na fungeni mwezi wa Ramadhani, toeni Zaka ya mali zenu kwa moyo mkunjufu, na fanyeni utiifu kwa viongozi wenu, basi mtaingia Pepo ya Mola wenu. *(Mu'jam Kabeer, juzuu ya 8, uk. 115, Hadithi 7535)*

## Hakuna Nabii mwingine kabisa baada yangu

10. Manabii عَلَيْهِمُ السَّلَام walikuwa wakitawala katika Bani Israil. Kila nabii anapofariki, nabii mwingine alikuwa akimrithi. (Lakini kumbukeni!) **Hakuna nabii mwingine kabisa baada yangu.** Hata hivyo, kutakuwa na makhalifa na watakuwa wengi. *(Bukhari, juzuu ya 2, uk. 461, Hadithi 3455)*

## Maelezo ya Hadithi

Hiyo ni kusema, katika zama zangu, hakuna nabii yeyote ambaye atakuwa khalifa wangu katika uhai wangu kama vile

Sayyiduna Musa عَلَيْهِ السَّلَام alipoenda kuleta Torati juu ya Toor, Haroon عَلَيْهِ السَّلَام akawa khalifa wake muda kwa siku chache. Na hakuna nabii yeyote ambaye anaweza kuwa khalifa wangu wa kudumu. Kwa hiyo, makhalifa wangu ni wafalme wa Dini yangu, na makhalifa wa kiroho ni Auliya na wanachuoni. *(Mirat, juzuu ya 5, uk. 346)*

11. Hakuna kilichobakia kutoka kwenye utume, isipokuwa habari njema tu. Maswahaba wakauliza kwa unyenyekevu: Ni zipi habari njema? akasema, 'Ndoto njema.' *(Bukhari, juzuu ya 4, uk. 404, Hadithi 6990)*

12. Hakuna utakaobakia katika Utume baada yangu ila ni habari njema. Hiyo ni, ndoto nzuri ambayo mtu aone mwenyewe au aonyeshwe mtu mwingine. *(Musnad Imam Ahmad Bin Hanbal, juzuu ya 9, uk. 450, Hadithi 25031)*

13. Hakika utume na unabii ulikwisha, kwa hivyo hakuna Mtume wala Nabii baada yangu. *(Tirmizi, juzuu ya 4, uk. 121, Hadithi 2279)*

14. Mimi ni Muhammad; Mimi ni Ahmad; Mimi ni Mtume wa Rehma; Mimi ni Mtume wa toba; Mimi ndiye Nabii wa Mwisho; Mimi ni Hashir; Mimi ni Mtume wa majihaad. *(Shamail-e-Tirmizi, uk. 215, Hadithi 361; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 657)*

*Un kay har Naam-o-Nisbat peh naami Durood*
*Un kay har Waqt-o-Halat peh lakhon salaam*

*(Hadaiq-e-Bakhshish)*

15. Mimi ni Ahmad; Mimi ni Muhammad na Muqaffa. *(Mu'jam Awsat, juzuu ya 1, uk. 622, Hadithi 2280)* Maana ya Muqaffa ni Aakhir-ul-Anbiya yaani mwisho wa Mitume. *(Al-Istazkaar li Ibn-e- 'Abdul Bir, juzuu ya 2, uk. 326)*

16. Sisi ni wa mwisho katika zama na wa kwanza Siku ya Kiyama. *(Bukhari, juzuu ya 1, uk. 303, Hadithi 876)*

## Ummah wa kwanza kuingia Peponi

Kwa maelezo ya Hadithi hii, mfasiri wa waislamu, Sayyiduna Imam Nawawi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameandika: Wanavyuoni wamesema, 'Maana ya Hadithi hii ni kwamba sisi ni wa mwisho kuja duniani, na wa kwanza wa kuingia Peponi. Kwa hiyo, Ummah huu utaingia Peponi kwanza kabla ya Ummah zote zilizotangulia. *(Sharh-e-Muslim-lil-Nawawi, juzuu ya 6, uk. 142)*

17. Sisi tutakuwa umma wa mwisho kuliko wote duniani na wa kwanza Siku ya Kiyama. Hukumu yetu itafanyika kwanza. *(Muslim, uk. 332, Hadithi 1982)*

## Mazungumzo Mafupi, Yenye Manufaa Mengi

18. Mwenyezi Mungu Mtukufu amenichagulia kamal-e-Ikhtisar (ufupilizo wenye ukamilifu) kwa hivyo sisi ni wa mwisho na siku ya Kiyama sisi ni wa mwanzo. *(Daarimi, juzuu ya 1, uk. 42, Hadithi 54, muhtasari)* Maana ya (kamal-e-ikhtisar) katika Hadithi ni kama ifuatavyo: Nilibarikiwa kwa ufupilizo wenye ukamilifu unaomaanisha maneno machache na maana nyingi zaidi. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 30, uk. 210)*

19. Hakika mimi nimetumwa niwe mwenye kuufungua mto wa rehema na kukamilisha unabii na utume. *(Shu'ab-ul-Iman, juzuu ya 4, uk. 308, Hadithi 5202; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 661)*

20. Mimi niliumbwa kabla ya manabii wote na kutumwa mwisho wa wote. *(Musnad Al-Shamiyeen, juzuu ya 4, uk. 34, Hadithi 2662)*

21. Mimi ndiye Mtume wa mwisho na nyinyi ni Umma wa mwisho. *(Ibn-e-Majah, juzuu ya 4, uk. 404, Hadithi 4077)*

## Sababu ya kuwa Nabii mwenye utukufu zaidi kuliko Manabii wote

Sayyiduna Sahl bin Salih Hamdani رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alimuuliza Sayyiduna

Imam Baqir رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه: Kama Mtume mtukufu صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alitumwa baada ya manabii wote عَلَيْهِمُ السَّلَام, Imekuaje Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alipata ubora juu ya nabii wote عَلَيْهِمُ السَّلَام? Mtume Mtukufu صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم Akasema: 'Siku ya Miithaaq (yaani siku ya ahadi) Mwenyezi Mungu Mtukufu alipowaleta katika wanadamu kizazi chao kutoka migongoni mwao, akawashuhudisha, na akasema: 'Je, mimi siye Mola wenu?' Kisha kabla ya wote Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akasema, 'بَلٰى' 'Kwani!' Ndiyo maana Mtume Mtukufu صَلَّى الله عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alipata ubora juu ya manabii wote عَلَيْهِمُ السَّلَام. Ingawa, alitumwa mwisho wa wote ulimwenguni. *(Khasais-e-Kubra, juzuu ya 1, uk. 7)*

*Qarnon badli Rasoolon ki hoti rehi*

*Chand badli ka nikla hamara Nabi*

*Kaya khabar kitnay taaray khilay chup ga`ye*

*Per na dubay na duba hamara Nabi*

*(Hadaiq-e-Bakhshish)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

22. (Sayyiduna) Adam عَلَيْهِ السَّلَام ndiye wa kwanza wa manabii wote, na (Sayyiduna) Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ni Mwisho wa Manabii. *(Al-Awail-lil-Tabrani, uk. 39, Hadithi 13)*

23. 'لَوْ كَانَ بَعْدِىْ نَبِيٌّ لَكَانَ عُمَرَبْنَ الْخَطَّابِ' Yaani kama kungelikuwa na

baada yangu kuna Nabii, angelikuwa Umar. *(Tirmizi, juzuu ya 5, uk. 385, Hadithi 3706)*

## Maelezo ya Hadithi

Katika maelezo ya hadithi hii, Imam Ahmad Raza Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه Amesema: Yaani umbile lake lilikuwa limekamilika kiasi kwamba lau mlango wa Utume haungefungwa, angeweza kuwa Mtume tu kwa rehma ya Mwenyezi Mungu Mtukufu, kwani hakuna anayestahiki mwenyewe kuwa mtume. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 29, uk. 373)*

24. Abuu Bakr رَضِىَ اللهُ عَنْهُ ni bora kuliko watu wote isipokuwa Manabii (na Mitume). *(Al-Kamil li Ibn-e- 'Adi, juzuu ya 6, uk. 484)*

## Kutakuwa na Manabii wa uongo 30 (thelathini)

25. Hivi karibuni kutakuwa na Manabii Kadhaab 30 (yaani, waongo wakubwa sana) katika Ummah wangu. Kila mmoja wao atadhani kuwa yeye ni nabii. Hata hivyo, mimi ni Khaatam-un-Nabiyyeen (yaani, Mtume wa Mwisho), na hakuna Nabii yeyote baada yangu. *(Abu Dawood, juzuu ya 4, uk. 132, Hadithi 4252)*

## Maelezo ya Hadithi

Katika maelezo ya Hadithi hii, Sayyiduna Mufti Ahmad Yaar

Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Hawa manabii 30 wa uwongo ni wale ambao watu waliwaamini kuwa ni manabii, na uharibifu wao ukaenea. Aina nyingine ya Mudda'i-e-Nabuwwat (yaani, wale wanaodai kuwa nabii) ambao watu hawakuamini walizungumza takataka na kufa. Wao ni wengi.

Sayyiduna Mufti Ahmad Yaar Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema zaidi: Tulikuja kujua kwamba Khaatam-un-Nabiyyeen maana yake ni Mtume wa Mwisho, kwani hakuna Mtume katika zama zake na baada yake. Ummah una maafikiano kuhusu maana hii. Yeyote anayesema kuwa maana yake si 'nabii wa mwisho', lakini kwa hakika, ni nabii wa kweli, huyo ni kafiri. *(Mirat, juzuu ya 7, uk. 219-220)*

26. Katika Ummah wangu watakuwa Kadhaab na Dajjal (waongo na wadanganyifu) wanne watakuwa wanawake, na mimi ni Nabii wa Mwisho, hakuna Nabii yeyote baada yangu. *(Mu'jam Kabeer, juzuu ya 3, uk. 169, Hadithi 3026)*

## Ubora wa Maula Ali

27. Wakati akienda kwenye Vita vya Tabuk Nabii Mtakatifu صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alimuacha Sayyiduna Ali رَضِیَ اللّٰهُ عَنْهُ Madinah, رَضِیَ اللّٰهُ عَنْهُ akasema kwa unyenyekevu, 'Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Unaniacha miongoni mwa wanawake

na watoto.’ Yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akasema, ‘Je, huridhii jambo hili kwamba ubaki hapa kama khalifa wangu kama Musa عَلَيْهِ السَّلَام alivyomuacha Haruon عَلَيْهِ السَّلَام kama khalifa wake alipokwenda kuzungumza na Mola wake Mtukufu. Hata hivyo, tofauti ni kwamba Haroon عَلَيْهِ السَّلَام alikuwa nabii. Na mimi tangu niwe Nabii, hakuna utume kwa mwingine. *(Muslim, uk. 1006, Hadithi 6218; Tirmizi, juzuu ya 5, uk. 407, Hadithi 3745)*

## Maelezo ya Hadithi

Mfasiri wa Bukhari, Sayyiduna Mufti Sharif-ul-Haq Amjadi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alisema: Wakati Sayyiduna Musa عَلَيْهِ السَّلَام alikwenda kwenye Mlima Toor ili kuleta Taurati, alimfanya Sayyiduna Haruon kwa muda عَلَيْهِ السَّلَام kuwa khalifa wake hadi kurudi kwake. Hilo liliisha baada ya kurejea kwake. Mfano huu ulidhihirisha kwamba Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alimuweka Sayyiduna Ali رَضِیَ اللهُ عَنْهُ kama khalifa wake kwa muda hadi kurejea kwake kutoka Tabuk. Ukhalifa huo ulikuwa tu kwa masuala ya usimamizi. *(Nuzha-tul-Qaari, juzuu ya 4, uk. 602)*

28. Ali anatokana na mimi kama vile Haroon anatokana na Musa (kwa kuwa yeye ni ndugu na Khalifa), lakini ‘لَا نَبِیَّ بَعْدِیْ’ hakuna nabii baada yangu. *(Tareekh-e-Baghdad, juzuu ya 7, uk. 463)*

29. Mimi ni Muhammad, Mtume Ummiyyi (yaani, Mtume ambaye hakujifunza kutoka kwa yeyote duniani) (alisema mara tatu), na 'لَا نَبِيَّ بَعْدِیْ' hakuna nabii baada yangu.

30. Mwenyezi Mungu Mtukufu aliniruzuku nilichotaka, lakini nikaambiwa kwamba hakuna Nabii yeyote baada yako. *(Al-Sunnah li Ibn-e-Abi 'Asim, uk. 303, Hadithi 1348)*

*Aye Khatam-e-Rusul, Makki Madani*

*Konayn mayn Tum sa ko`yi nahin*

## Umesema ukweli

31. Malaika watamuuliza aliyekufa kaburini, 'Nani mola wako?' Dini yako ni ipi?' 'Nabii wako ni nani?'. Anasema, 'Mola wangu ni Allah, ambaye hana mshirika; na Dini yangu ni Uislamu; na Mtume wangu ni (Sayyiduna) Muhammad (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم); naye ndiye Nabii wa Mwisho. Malaika husema, 'Umesema ukweli.' *(Zikr Al-Maut ma' Mausu'ah lil Imam Ibn Abi Al-Dunya, juzuu ya 5, uk. 474, Hadithi 254; Sharh-us-Sudoor (Urdu) uk. 130)*

## Tafsiri ya ndoto

32. Kufasiri ndoto ya Sayyiduna ibn Ziml رَضِیَ اللهُ عَنْهُ akasema: Ama yule ngamia jike uliyemwona katika ndoto, na mimi

nimempanda, inaashiria Siku ya Kiyama na kwamba hakutakuwa na Nabii yeyote baada yangu, wala hautakuwa na Ummah baada ya Ummah wangu. *(Dalail-un-Nubuwwah-lil-Bayhaqi, juzuu ya 7, uk. 38)*

## Nur (mwanga) itakuwa mbele yao

33. Bila ya shaka yoyote Siku ya Kiyama Mwenyezi Mungu Mtukufu ataita Sayyiduna Nuh عَلَيْهِ السَّلَام na watu wake kabla (hajamuita) mwengine na kusema: 'Je, mulimjibu nini Nuh?' Watasema: 'Nuh (عَلَيْهِ السَّلَام) hajatulingania kwako, wala hajatufikishia ujumbe wako, wala hajatunasihi, wala hakueleza hukumu yoyote ya kheri au mbaya.' Sayyiduna Nuh عَلَيْهِ السَّلَام atasema, 'Ilahi! Niliwalingania kwenye haki kwa namna ambayo ilienea miongoni mwa wote watangulizi na warithi mmoja baada ya mwingine mpaka huo (wito) ukamfikia Mtume wa Mwisho (Sayyiduna) Ahmad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Waliiandika na kuisoma (yaani, ilitajwa ndani ya Qur'ani Tukufu iliyoandikwa na kusomwa), na wakaiamini na kuithibitisha.' Mwenyezi Mungu Mtukufu atasema, 'Mwiteni Ahmad. (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم) na Umma wa Ahmad.' Kisha Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم na Ummah wake utawasili kwenye baraza la Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa namna ambayo Nur itakuwa imewatangulia. Watatoa ushuhuda wa Nuh (عَلَيْهِ السَّلَام)

(yaani, wataunga mkono.) *(Al-Mustadrak, juzuu ya 3, uk 415, Hadithi 4066; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya15, uk. 690)*

## Viumbe vyote vitamwita Mtume wa Mwisho Siku ya Hukumu

34. Watanijia watangulizi na warithi na kusema, 'Ewe Mtume! Wewe ni Mtume wa Mwenyezi Mungu Mtukufu na Khaatam-ul-Anbiya yaani, Mtume wa Mwisho, tuombee.' *(Bukhari, juzuu ya 3, uk.260, Hadithi 4712, muhtasari)*

يَا شَفِيْعَ الْوَرٰى سَلَامٌ عَلَيْك     يَا نَبِيَّ الْهُدٰى سَلَامٌ عَلَيْك

خَاتَمَ الْاَنْبِيَاء سَلَامٌ عَلَيْك     سَيِّدَ الْاَصْفِيَاء سَلَامٌ عَلَيْك

## Kama Muhammad Asingekuwepo, Nisingekuumba Wewe

35. Pale (Sayyiduna) Adam عَلَيْهِ السَّلَام alifanya kosa la hukumu (Khata Ijtihadi), aliinua kichwa chake kilichobarikiwa kuelekea 'Arsh na kwa unyenyekevu akamwambia Allah Mtukufu, 'Ewe Allah! Ninakuomba kukupa Wasilah/ukatikati wa Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kunisamehe.' Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema, 'Ewe Adam! Umemjuaje Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم? Hata hivyo,

sijamuumba bado. Sayyiduna Adam عَلَيْهِ السَّلَام akasema, 'Ewe Mwenyezi Mungu! Uliponiumba kwa uwezo wako, niliinua kichwa changu nikaona 'لَآاِلٰهَ اِلَّا اللّٰهُ مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ' imeandikwa kwenye miguu ya Arsh yako, kwa hiyo nikajua kwamba ni lazima uliemjumlishe jina Lake kwa lako ni kipenzi Kwako kuliko walimwengu wote na ana heshima kubwa Kwako." Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema, 'Ewe Adam! Umesema ukweli. Bila shaka yoyote, yeye ni kipenzi kwangu kuliko walimwengu wote. Uliponiomba kunipa Wasilah ya Muhammad, nilikusamehe makosa yako. 'وَلَوْلَا مُحَمَّدٌ مَا خَلَقْتُكَ' yaani; **Kama Si Muhammad Kuwepo, Nisingekuumba Wewe.** Kuna nyongeza katika riwaya ya Tabarani: Naye ni Mtume wa mwisho miongoni mwa kizazi chako, na Ummah wake ni Umma wa mwisho miongoni mwa kizazi chako. *(Mu'jam Sagheer Juzz Saani, uk. 82; Fatawa Razawiyyah, juzuu. 15, uk. 633)*

*Woh jo na thay tau kuch na tha, Woh jo na hon tau kuch na ho*

*Jaan hayn Woh jahan ki, jaan hay tau jahan hay*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

36. Sayyiduna Adam عَلَيْهِ السَّلَام alipotua India kutoka peponi, alikuwa na wasiwasi. Jibril akashuka na kutoa Azan. Jina lililobarikiwa lilipokuja, Sayyiduna Adam عَلَيْهِ السَّلَام akauliza, 'Muhammad ni nani?' Akasema, 'Mtume wa mwisho miongoni mwa kizazi chako.' *(Ibn-e- 'Asakir, juzuu ya 7, uk. 437; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 640)*

## Imetajwa katika Taurati

37. Ilipoteremshwa Taurati juu ya (Sayyiduna) Musa عَلَيْهِ السَّلَام, alikuta ndani yake utajo wa Ummah huu, kwa unyenyekevu alimwambia Mwenyezi Mungu Mtukufu, 'Ewe Mola wangu! Nimekuta utajo wa Ummah ndani yake ambao kwamba ni wa mwisho katika zama na wa kwanza katika daraja. Basi, ufanye Ummah wangu.' Mwenyezi Mungu Mtukufu akasema, 'Huu ni Umma wa Ahmad.' *(Dalail-un-Nubuwwah li Abi Na'eem, uk. 33, Hadithi 31; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 633)*

*Kitab-e-Sayyiduna-e-Musa mayn wasf hayn un kay*
*Kitab-e-'Isa mayn un kay fasanay aye hayn*
*Unheen ki na't kay naghmayn Zaboor say sun lo*
*Zaban-e-Quran peh un kay taranay aye hayn*

*(Saman-e-Bakhshish, uk. 125)*

## Wa kwanza na wa mwisho

38. Mwenyezi Mungu Mtukufu alipomuumba (Sayyiduna) Adam عَلَيْهِ السَّلَام na akaonyeshwa kizazi chake, akawaona wametofaotiana katika ubora, na aliposhuhudia Nuru/mwangaza mkubwa na mkali mwishoni mwao, alimuuliza Mwenyezi Mungu Mtukufu, 'Ewe Mwenyezi Mungu Mtukufu! Huyu ni nani?' Akasema, 'Yeye ni mwanao, Ahmad.' Yeye ndiye wa kwanza, na ndiye wa mwisho, na ndiye muombezi wa kwanza, na ndiye wa kwanza ambaye uombezi wake utakubaliwa. *(Dalail-un-Nubuwwah-lil-Bayhaqi, juzuu ya 5, uk. 483; Kanz-ul-Ummal, juzuu ya 11, uk. 197, Hadithi 32053; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 634)*

*Zaat hoyi intikhab wasf huway la-jawab*
*Naam huwa Mustafa tum peh karoron durood*

## Nabii Wa Kwanza Na Wa Mwisho

39. Sayyiduna Abu Hurayrah رَضِىَ اللهُ عَنْهُ alisema: (Katika usiku wa Mi'raj) wakati Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alikutana na Manabii عَلَيْهِمُ السَّلَام katika mbingu, wote wakamuhimidi na kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, na mwisho Mtume wa Mwisho, Muhammad صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akasema, 'Nyinyi nyote mumemhimidi Mwenyezi Mungu, sasa mimi

nitamhimidi: Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, aliyenituma niwe rehema kwa walimwengu wote; na amenituma mimi nihubirie habari njema na maonyo kwa watu wote; na ikateremshwa juu yangu Qurani Tukufu, ambayo ina utajo wazi wa kila kitu; na akaufanya Ummah wangu kuwa Ummah bora kuliko Ummah zote zilizojitokeza miongoni mwa watu; na kuifanya wa kwanza na wa mwisho; na akaninyanyulia utajo wangu; na kuanza utume kutoka kwangu; na kuitimiza juu yangu.' Aliposikia hayo, Sayyiduna Ibrahim Khalilullah عَلَيْهِ السَّلَام aliwaambia manabii wote, 'Kwa sababu ya sifa hizi, Muhammad (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم) ni bora kuliko nyinyi nyote.' Kisha Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akaenda Sidrah-tul-Muntaha. Kisha Mwenyezi Mungu Mtukufu akazungumza naye na kusema hivi vilevile, 'Nimekuumba kabla ya Mitume wote, na nikakutuma mwisho wa Mitume wote, na nikakufanye wewe ni Faatih na Khaatam (yaani, wa kufungua na wa mwisho). *(Tafseer Tabri, juzuu ya 8, uk. 8-9, Hadithi 22021; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 637)*

*Tum ho awwal, Tum ho aakhir, Tum ho Baatin, Tum ho Zaahir*
*Haq nay bakhshay hayn yeh asma,* صَلَّى اللهُ عَلَيْكَ وَسَلَّم

## ‘اَنَا لَهَا’ Itasikika kwenye midomo ya Mtume wangu

40. Watu watakapokata tamaa juu ya uombezi kutoka kwa Mitume wote عَلَيْهِمُ السَّلَام, watakwenda kwa (Sayyiduna) ‘Isa Ruhullah عَلَيْهِ السَّلَام, kufanya maombi ya maombezi. Atasema, ‘Siwezi kufanya kazi hii ila (Sayyiduna) Muhammad Khaatam-un-Nabiyyeen (yaani, mwisho wa Mitume wote) صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم yuko hapa. Watu watakapokuja kwangu na kuomba uombezi, nitasema ‘اَنَا لَهَا’ yaani, mimi niko kwa ajili ya hii (kazi). *(Musnad Abu Ya’la, juzuu ya 2, uk. 368, Hadithi 2324; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 639)*

*Kaheen gay aur Nabi ‘اِذْهَبُوْا اِلٰى غَيْرِى’*
*Mayray Huzoor kay lab per ‘اَنَا لَهَا’ ho ga*

## Ufafanuzi wa mashairi ya Hassan

Siku ya Hukumu ambapo watu wataomba uombezi kwa Mitume wote watasema, ‘Nendeni kwa mtu mwingine asiyekuwa mimi.’ Watakapokata tamaa kwa wote, watamjilia Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم na kuomba maombezi. Atasema, ‘Mimi niko kwa ajili ya kazi hii.’

*Day day shafa’at ki khayraat mujhay khayr say*
*Roz-e-Qiyamat bakhshuwa, aye Aakhiri Nabi (ﷺ)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب      صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sijakuficha chochote isipokuwa...

Taba'i, Mtakatifu Sayyiduna Ka'b-ul-Ahbar رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه Alisema: Baba yangu alikuwa na elimu zaidi miongoni mwa wale waliokuwa na elimu ya Taurati. Yoyote ambayo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliyateremsha juu ya Sayyiduna Musa عَلَيْهِ السَّلَام, hakuna aliyejua zaidi ya baba yangu. Hakunificha chochote kuhusu elimu yake. Ulipofika muda wake wa mwisho, aliniita na kusema, 'Ewe mwanangu! Unajua ya kwamba sikukuficha chochote chini ya ujuzi wangu, isipokuwa nimehifadhi kurasa mbili. Ndani yake ametajwa Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ambaye muda wake wa kuwasili umefika. Sijakujulisha kuhusu kurasa hizi mbili kwa kuogopa kwamba anaweza akatokea mtu (ambaye atajidai kuwa nabii) nawe usije ukamfuata. Kifua hiki kiko mbele yako. Nimeweka hizo kurasa ndani yake na kuweka udongo juu. Usione kurasa hizo kwa sasa. Wakati Mtume huyo (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم) atakapokuja na Mwenyezi Mungu Mtukufu akakuhurumia, utamfuata mwenyewe. Baada ya kusema hayo alifariki. Tulipomaliza kumzika, nilikuwa na hamu ya kuona kurasa hizo zaidi kuliko kitu kingine chochote. Nilipofungua kifua na kutoa zile kurasa, nilichokiona ni kwamba kimeandikwa:

مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ خَاتَمُ النَّبِيّٖنَ لَا نَبِيَّ بَعْدَهٗ مَوْلِدُهٗ بِمَكَّةَ وَ مُهَاجَرُهٗ بِطَيْبَةَ

Yaani, Muhammad ni Mtume wa Mwenyezi Mungu, Nabii wa Mwisho, hakuna Nabii yoyote baada yake, kuzaliwa kwake ni Makka, na atahamia Madina. *(Khasais-e-Kubra, Juzuu ya 1, uk. 25)*

*Ba'd Aap kay hergiz na aye ga Nabi naya*
*Wallah! Iman hay Mayra, Aye Aakhiri Nabi (ﷺ)*

*Hay dast bastah sar jhuka ker 'arz Sayyidi!*
*Tau khuwab mayn jalwah dikha, Aye Aakhiri Nabi (ﷺ)*

*Aalai`shon say pak ker kay mayray dill mayn tau*
*Aa-ja sama-jaa ghar bana, Aye Aakhiri Nabi (ﷺ)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

# Maneno Matano ya Maswahaba na Taba'een

## 1. Maandishi kati ya mabega mawili

Swahaba wa Mtume Mtukufu, Sayyiduna Jabir bin Abdullah رَضِىَ اللهُ عَنْهُ akasema, 'Imeandikwa kati ya mabega mawili ya Sayyiduna Adam Safiullah عَلَيْهِ السَّلَام 'مُحَمَّدٌ رَّسُوْلُ اللّٰهِ خَاتَمُ النَّبِيّٖن' yaani, Muhammad (صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم) ni Mtume wa Mwenyezi Mungu na

Nabii wa Mwisho.’ *(Tareekh Dimashq, juzuu ya 2, uk. 137; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 634)*

## 2. Kama Asingekuwepo, Hakuna Kitu chochote Kingekuwapo

Swahaba wa Mtume Mtukufu, Sayyiduna Salman Farsi رَضِیَ اللهُ عَنْهُ amesema, ‘Sayyiduna Jibril Amin عَلَيْهِ السَّلَام alikuja na kumwambia Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, ‘Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu! Mola wako anasema: Hakika Mimi nimekutimizia Mitume juu yako (yaani wewe ni Nabii wa Mwisho) na sikumuumba aliye mtukufu zaidi yako kwangu. Jina lako nimeliunganisha na langu, ili popote nitakapotajwa wewe pia utajwe. Hakika, Niliumba ulimwengu na watu wanaoishi katika ulimwengu, ili niwaonyeshe heshima yako, daraja lako na cheo chako kwangu. Kama usingekuwepo, nisingeliumba mbingu, dunia na vyote vilivyomo. *(Tareekh Dimashq, juzuu ya 2, uk. 136-137; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 636)*

*Hay unheen kay dam qadam ki bagh-e-‘aalam mayn bahar*
*Woh na thay ‘aalam na tha, gar woh na hoon ‘alaam nahin*

## Ufafanuzi wa ushairi wa Raza

**Uzuri wote na uzuri wa ulimwengu unatokana na** Nabii wa

Mwisho wa Mwenyezi Mungu (صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم). Ikiwa Nabii wangu Mpendwa صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم hangelikuja ulimwenguni, ulimwengu huu usingekuwepo.

*Aye keh tayra Wujood hay, wajah-e-qarar-e-do-jahan*

*Aye keh tayri numood hay, Zeenat-e-Bazm-e-Kai`naat*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## 3. Ujumbe kwa Sayyiduna Ibrahim عَلَيْهِ السَّلَام

**Mtakatifu** Taba'i, Sayyiduna Amir Sha'bi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Sahifa ambazo Mwenyezi Mungu Mtukufu aliziteremsha juu ya (Sayyiduna) Ibrahim (Khalilullah عَلَيْهِ السَّلَام) pia zilijumuisha yafuatayo: Hakika kutakuwa na kabila baada ya kabila katika kizazi chako hadi Mtume Ummi (yaani, Mtume ambaye hakujifunza kutoka kwa yeyote duniani) Khaatam-ul-Anbiya. (صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم) atakuja. *(Al-Tabqaat Al-Kubra li Ibn-e-Sa'd, juzuu ya 1, uk. 130; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 635)*

Bwana wangu, A'la Sayyiduna رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه ameandika:

*Aisa Ummi kis liye minnat kash-e-ustad ho*
*Kiya kifayat us ko 'اِقْرَاْ رَبُّكَ الْاَكْرَمْ' nahih*

## Ufafanuzi wa ushairi wa Raza

Mwenyezi Mungu Mwenyewe alimfundisha Mtume wa Mwisho, ambayo imetajwa katika juzuu ya 30 katika Surah ‘Alaq. Na kwa vile Mwenyezi Mungu Mtukufu mwenyewe amemfundisha, kwanini abebeshwe mzigo wa kufanyiwa wema na mwalimu yoyote wa ulimwengu. Na kuwa kwake 'Ummi' ni miujiza kubwa kwamba hakujifunza kutoka kwa mtu yeyote, lakini alipata elimu zote za ulimwengu.

## 4. Ufunuo Juu Ya Sayyiduna Ash’iya عَلَيْهِ السَّلَام

Mtakatifu Taba’i, Sayyiduna Wahb bin Munabbah رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه, alisema: Mwenyezi Mungu Mtukufu alimteremshia wahyi Mtume wake kipenzi, Sayyiduna Ash’iya عَلَيْهِ السَّلَام kwamba nitamtuma Mtume Ummi, ambaye kupitia kwake nitafungua masikio ya uziwi, nyoyo zilizoghafilika, na macho ya vipofu. Kuzaliwa kwake ni Makka, mahali pa kuhama ni Madina, na ufalme wake uko katika ‘Syria’. Hakika nitaufanya Ummah wake kuwa bora na mkubwa kuliko Ummah wote uliodhihiri kwa watu. Nitakamilisha vitabu vingine katika kitabu chao, Sheria nyinginezo juu ya Sheria yao, na dini nyinginezo katika dini yao. *(Dalail-un-Nubuwwah li Abi Na’eem, uk. 36, Hadithi 33; Al-Khasais-ul-Kubra, juzuu ya 1, uk. 23; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 635)*

*Kaleem-o-Naji Maseeh-o-Safi Khaleel-o-Razi Rasool-o-Nabi*
*'Ateeq-o-Wasi Ghani-o-Ali Sana ki zaban tumharay liye*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Maelezo ya Ufalme wa Syria

Enyi wapenzi wa Mtume wa Mwisho! Hadithi ambayo imetajwa hivi punde pia inaeleza ufalme wa Mtume wetu Mpenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم itakuwa Syria. Katika suala hili, hapa nawasilisha lulu ya Madani kutoka Kwa Fatawa Razawiyyah Sharif kwa wapenzi wa maswahaba na Ahl-e-Bayt: Bwana wangu, A'la Hazrat رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه. amesema, 'Sayyiduna Ameer Mu'awiyah رَضِىَ اللهُ عَنْهُ ndiye mfalme wa kwanza wa uislamu (yaani ufalme wa Mtume Muhammad). Imeashiriwa hata katika Taurati takatifu: 'مُوْلِدُهٗ بِمَكَّةَ وَ مُهَاجَرُهٗ طَيْبَةَ وَ مُلْكُهٗ بِالشَّامِ' yaani Nabii Yule wa Mwisho صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم atazaliwa Madina, atahamia Madina, na ufalme wake utakuwa Shamu.' Kwa hiyo, ingawa Ameer Mu'awiyah رَضِىَ اللهُ عَنْهُ ndiye aliyekuwa mfalme lakini ufalme wake ni wa nani! Ni wa Mtume Muhammad. *(Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 29, uk. 357)*

*Har Sahabi'ay Nabi! …… Jannati Jannati*
*Sab Sahabiyat bhi! …… Jannati Jannati*

*Char Yaraan-e-Nabi …… Jannati Jannati*
*Sayyiduna-e-Siddique bhi …… Jannati Jannati*

*Aur Umar Farooq bhi …… Jannati Jannati*
*Usman-e-Ghani …… Jannati Jannati*

*Fatimah aur Ali! …… Jannati Jannati*
*Hayn Hassan aur Hussain bhi…… Jannati Jannati*

*Walidayn-e-Nabi! …… Jannati Jannati*
*Har zoja'ay Nabi! …… Jannati Jannati*

*Aur Abu Sufiyan bhi!…… Jannati Jannati*
*Hayn Mu'awiyyah bhi! …… Jannati Jannati*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## 5. Uteremsho Juu Ya Sayyiduna Yaaqoob عَلَيْهِ السَّلَام

Mtakatifu Taba'i, Sayyiduna Muhammad bin Ka'b Qurazi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alisema: Mwenyezi Mungu Mtukufu aliteremsha wahyi juu ya Sayyiduna Yaaqoob عَلَيْهِ السَّلَام: Nitaendelea kutuma wafalme na manabii عَلَيْهِمُ السَّلَام kutoka kwa kizazi chako hadi kwamba nitamtuma Mtume Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, ambaye Ummah wake utajenga Bayt-ul-Muqaddas, naye ni 'Mtume wa Mwisho', na jina lake ni 'Ahmad'. *(Al-Tabqat Al-Kubra li Ibn-e-Sa'd, juzuu ya 1, uk. 129; Fatawa Razawiyyah, juzuu ya 15, uk. 635)*

## Kauli Mbiu Za Mwisho Wa Utume

| |
|---|
| Muhammad ndiye Mustafa<br>"Mwisho wa Manabii wote" |
| Ahmed ndiye Mujtaba<br>"Mwisho wa Manabii wote" |
| Mpendwa wa Amna<br>"Mwisho wa Manabii wote" |
| Mfalme wa walimwengu wote wawili<br>"Mwisho wa Manabii wote" |
| Kiongozi wa Manabii<br>"Mwisho wa Manabii wote" |
| Kipenzi cha Mwenyezi Mungu<br>"Mwisho wa Manabii wote" |
| Mwombezi mkuu<br>"Mwisho wa Manabii wote" |
| Tumaini la wenye dhambi<br>"Mwisho wa Manabii wote" |
| Imani ya Fatimah<br>"Mwisho wa Manabii wote" |

| |
|---|
| Imani ya Aisha<br>“Mwisho wa Manabii wote” |
| Imani ya Maswahaba wote<br>“Mwisho wa Manabii wote” |
| Imani ya familia iliyobarikiwa<br>“Mwisho wa Manabii wote” |
| Imani ya Ghaws-e-Pak<br>“Mwisho wa Manabii wote” |
| Watakatifu pia wamesema<br>“Mwisho wa Manabii wote” |
| Wazee na vijana walisema<br>“Mwisho wa Manabii wote” |
| Hata kila mtoto alisema<br>“Mwisho wa Manabii wote” |
| Imani ya Raza<br>“Mwisho wa Manabii wote” |
| Kauli mbiu ya Attar<br>“Mwisho wa Manabii wote” |

## Mpe mtu mwingine kijitabu hiki baada ya kukisoma

Pata thawabu kwa kusambaza vijitabu hivi vilivyochapishwa vya Maktaba-tul-Madīnaĥ na vijitabu vyenye lulu vya Madanī kwenye hafla za harusi, mazishi, Ijtima'āt, za harusi, maandamano ya Mīlad n.k. Jenga mazoea ya kuweka vijitabu dukani kwako ili kuvizawadia. kwa wateja wako kwa nia ya kuvuna zawadi. Tuma angalau kijitabu kimoja chenye Msukumo wa Sunnaĥ au kijitabu chenye lulu za Madanī kwa kila nyumba katika mtaa wako kwa usaidizi wa watoto au watengeneza karatasi, ukiongeza juhudi za kufikisha wito wa kuelekea kwenye haki na kupata thawabu kubwa.

# Burden of (keeping an unowned) date

Some people were sitting in Bayt-ul-Maqdas after offering Nafl Salah. A pious man said: Ibrahim Bin Adham has been deprived of the pleasure of worship for 40 days. Hearing this, he رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه said: Hadrat! You are telling the truth, but for what reason was I deprived of it? The pious man said: You had bought dates on a such-and-such day in Basra. A date belonging to the seller was lying there. You picked it up thinking it was yours (that date is the reason for your deprivation of the pleasure of worship). Hadrat Ibrahim Bin Adham رَحْمَةُ اللهِ عَلَيْه travelled to Basra to have that date forgiven and got it forgiven. *(Tazkra-tul-Awliya`, vol. 1, p. 102, summarised)*

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran
Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan
UAN: +92 21 111 25 26 92 | Ext: 7213
Web: www.maktabatulmadinah.com | E-mail: feedback@maktabatulmadinah.com